

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

JULAI / AGOSTI 2013

MUDA: Saa 2½

## MTIHANI YA UTATHMINI WA PAMOJA WILAYA YA KIKUYU

HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KENYA (K.C.S.E)

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: Saa 2½

### MAAGIZO

1. Jibu maswali manne pekee
2. Swali la kwanza ni la lazima
3. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani:  
Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Fasihi simulizi
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

## SEHEMU YAA: USHAIRI

### SWALILA LAZIMA.

#### 1. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

**Hayawani** nondokeya, nondokeya nenda mbali  
melaniwa huna haya, leo haja kukabili.  
kimbiya nenda waya, upindo wako usuli?  
Ubakaji haini.

Watoto waulizani, changudoa mekushinda?  
Umezua vya uhuni, kuyachafua makinda  
Pinga kama si punguani, adilifu mekushinda  
Ubakaji haini.

Wahanyahanya yayaya, mitaani patupatu  
Matendoyo kubwayaya, **umewasinya** wenetu  
Nairobi na Siaya, kote kote lithubutu  
Ubakaji haini.

Jogoo kuparagia, kifaranga ni halali?  
Ukimwi wawapatia, huna akili kamili  
Nakutungia sheria, takufunga ukubali  
Ubakaji haini.

#### Maswali

- a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)
- b) Shairi hili ni la bahari gani? Thibitisha. (alama 2)
- c) Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili. (alama 2)
- d) Taja na ueleze tamathali mbili za lugha alizotumia mtunzi. (alama 2)
- e) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- f) Taja matendo yoyote matatu mabaya ya anayesemwa. (alama 3)
- g) Eleza jinsi mshairi alivyotumia uhuru wake wa utunzi. (alama 4)
- h) Eleza maana kimuktadha ya maneno yafuatayo  
(i) Hayawani (alama 1)  
(ii) Umewasinya (alama 1)

## SEHEMU YAB: RIWAYA

### S.A. MOHAMMED: *Utengano*.

#### Jibu swali (2) au (3)

2. Ndoto na nyimbo ni ufundi wa kisimulizi unaojikita katika misingi ya taswira katika *Utengano*.  
Huku ukianza kwa kufafanua taswira, eleza jinsi mwandishi anavyozitumia kufanikisha malengo yake ya usimulizi. (alama 20)

3. “Shoga Futoni ni Futoni kweli, mambo yake ni mfutofuto, hakuna mtaji mkubwa hata hivyo kwa mimi na wewe .....”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Eleza njia alizotumia kujipatia riziki mnenewa zilivyomtia mashakani. (alama 10)
- c) Eleza jinsi mnenewa hakubadilisha maisha yake. (alama 6)

### SEHEMU YA C: TAMTHILIA

**TIMOTHY M. AREGE: *Mstahiki Meya.***

**Jibu swali (4) au (5)**

4. Huku ukirejelea tamthilia ya *Mstahiki Meya*, fafania malengo manne ya mwandishi. (alama 20)
- Au
5. “..... tafadhali mwanangu, nihurumie ..... Ni hiki tu. Sina chengine ..... Niokolee mwanangu.”
- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
- b) Fafania kwa kutolea mifano sifa zozote tatu za mzungumziwa. (alama 6)
- c) Watu wa tabaka la mzungumziwa walikuwa wakipitia katika masaibu gani? Fafania kwa kutolea mifano. (alama 8)
- d) Eleza hatima ya mrejelewa. (alama 2)

### SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

**KEN WALIBORA na SAID A. MOHAMED: *Damu Nyeusi.***

**Jibu swali (6) au (7)**

6. Huku ukirejea hadithi zozote nne katika *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, onyesha namna swala la ndoa linavyojitokeza katika jamii mbalimbali. (alama 20)
- Au
7. ‘Alaa! Hivi ndivyo alivyo mke wangu! Hivyo mimi hanioni kuwa mume kwake maadamu sifanyi kazi!’
- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
- b) Fafania sifa zozote tatu za mlalamishi. (alama 6)
- c) Kwa mujibu wa hadithi hii, ni zipi sifa za mume mzuri? (alama 6)
- d) Mke wa mlalamishi alikuwa na imani gani juu ya ndoa? (alama 4)

### SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. a) Mivigha ni nini? (alama 2)
- b) Fafania sifa zozote sita za mivigha. (alama 12)
- c) Mivigha ina majukumu yapi katika jamii? (alama 6)